

Haki na Majukumu ya Mzazi Asiyelea Noncustodial Parent's Rights and Responsibilities

Divisheni ya Kuwasaidia Watoto (DCS):

1. Huanzisha na kutekeleza maagizo ya msaada wa watoto na majukumu ya usaidizi wa matibabu.
2. Huhakiki maagizo ya msaada wa watoto kwa urekebisho unaowezekana.
3. Hupokea, kurekodi, na kusambaza malipo ya kuwasaidia watoto kupitia Rajisi ya Msaada ya Jimbo la Washington (WSSR).

Mzazi Asiyelea

Wewe ni mzazi asiyelea. Mzazi asiyelea ni baba aliyemzaa, au baba aliyekubaliwa kumchukua mtoto, mama aliyemzaa, au mama aliyekubaliwa kumchukua mtoto ambaye lazima atoe usaidizi wa kifedha kwa watoto wanaomtegemea. Sheria za jimbo na serikali zinatekeleza jukumu hili.

Malipo ya Kuwasaidia Watoto

Kwa kawaida, utalazimika kulipa msaada wa watoto. Baada ya DCS kukupa ilani inayokuhitaji ulipe msaada wa watoto, DCS haitaingiza pesa kwenye akaunti yako kwa malipo tu yaliyotumwa kwa mtu mwingine yoyote zaidi ya WSSR, mahakama nyingine ya jimbo au chombo cha kuwasaidia watoto, au mahakama ya kabila au chombo cha kuwasaidia watoto. DCS haitaingiza pesa kwenye akaunti yako kwa pesa iliyolipwa moja kwa moja kwa upande mwingine wa agizo la msaada isipokuwa pesa ikiwa imelipwa kutoka kwa wakala kwa mafao yenye kujitegemea, kama vile Idara ya Usalama wa Jamii, Idara ya Kazi na Viwanda, au Idara ya Mambo ya Askari wastaafu kwa lengo la deni la msaada wa watoto.

1. Elezea DCS mara moja kama jimbo lingine au chombo cha kabila cha msaada wa watoto au mahakama ya serikali ya ya kabila itakuomba uwalipe malipo ya msaada wa watoto.
2. Usitume malipo kwa mtu mwingine kando na anwani ya WSSR iliyoorodheshwa hapa chini isipokuwa kama DCS ikueleze kwa kuandika kwamba imefunga kesi yako.

Lazima ulipe malipo yote ya usaidizi kwa Sajili ya Msaada ya Jimbo la Washington (WSSR). Unaweza kulipa kwa kutumia mbinu zozote zifuatazo:

1. Kipunguzo cha malipo. Maagizo mengi ya msaada huwezesha DCS kukusanya usaidizi kwa kupunguza malipo au uhitaji malipo kupitia WSSR. Kama agizo lako linawezesha DCS kufanya hivyo, DCS itajaribu kukusanya msaada kwa matoleo ya malipo.
2. Cheki ya kibinafsi, hawala ya fedha, cheki iliyoidhinishwa, au cheki ya keshia. Tuma cheki zote na malipo ya hawala ya fedha kwa:

WASHINGTON STATE SUPPORT REGISTRY
PO BOX 45868
OLYMPIA WA 98504-5868

3. Hawili ya Fedha Kielektroniki (EFT). EFT huruhusu matoleo ya moja kwa moja ya malipo ya msaada kutoka kwenye akaunti ya cheki au ya akiba kila mwezi. Kwa maelezo zaidi kuhusu, piga sima 800-468-7422.
4. Wavuti. Malipo ya wavuti huruhusu matoleo ya malipo ya msaada kutoka kwenye akaunti ya cheki au ya akiba. Kwa maelezo zaidi, tembelea tovuti ya DCS, <https://secureaccess.wa.gov>.
5. Kadi ya Mkopo au ya Matumizi. Kwa maelezo zaidi, tembelea tovuti ya DCS, <https://www.dshs.wa.gov/esa/division-child-support/creditdebit-card-payments>.

Kama benki yako itarudisha moja ya cheki zako au ishindwe kukubali EFT au malipo ya wavuti kwa sababu ya fedha kutokuwepo, DCS itakubali malipo ya mustakabali na pesa taslimu tu, hawala ya fedha, cheki ya keshia, cheki iliyoidhinishwa, au kipunguzo cha malipo.

Jumuisha nambari ya kesi yako na nambari ya akaunti **IN** _____ kwenye malipo na mawasiliano yote.

DCS haitatoa fedha kwenye akaunti yako kwa malipo yaliyotumwa kwa mtu yeyote kando WSSR, mahakama ya kikabila au chombo cha usaidizi wa watoto, au mahakama nyingine ya jimbo au chombo cha usaidizi wa watoto. DCS haitatoa fedha kwenye akaunti yako kwa fedha zilizolipwa moja kwa moja kwa mhusika mwingine kwenye agizo hilo la msaada.

Kama una sababu za kisheria za kutotoa msaada wa kifedha kwa watoto wako au kama DCS ilikuhusisha kimakosa katika mchakato huu, arifu DCS mara moja.

Ikiwa DCS itakufahamisha kwamba tunasitisha kwa muda ukusanyaji wa deni lako la msaada, deni lako linaweza kuwa ni lenyekukusanywa siku za mbele. DCS itakufahamisha kabla ya kuchukua uamuzi huu.

Ikiwa umefungwa au umehukumiwa kifungo cha zaidi ya miezi sita jela, gerezani, au kituo cha kurekebisha tabia, agizo lako la matunzo ya watoto linaweza kupunguzwa kwa muda (kushushwa) kuwa \$10 kwa mwezi kwa kila agizo la matunzo ya watoto. Wewe, mzazi anayelea, au DCS inaweza kuomba punguzo. Ikiwa punguzo linahusika kwa suala lako, utapata arifa kutoka kwa DCS inayoelezea vigezo vya punguzo na haki ya kila mtu ya kuomba usikilizaji wa shauri ikiwa hakubaliani na jambo hili. Kiasi hicho kitaongezeka hadi 50% ya agizo la matunzo katika mwezi wa nne baada ya kuachiwa kwako, na kitaongezeka tena hadi 100% ya kiasi halisi mwaka mmoja baada ya kuachiwa kwako.

Majukumu ya Msaada wa Matibabu

Kama agizo lako la msaada linahitaji utoe bima ya afya kwa watoto wako, DCS itachukua hatua ili kutekeleza jukumu lako. Kama agizo lako la msaada linakuhitaji kulipa pesa taslimu za msaada wa matibabu, DCS itaweka kiwango cha dola unachohitajika kulipa na itakusanya kiwango hicho.

1. Elezea DCS mara moja kama kuna kitu chochote kitakachobadilika kuhusiana na bima yako ya afya kwa watoto waliotajwa kwenye agizo lako la msaada.
2. Pesa taslimu za msaada wa matibabu zinajumuisha kiwango kinachofaa cha gharama za matibabu ambazo hazijafidiwa na mgao wa pesa za matibabu (malipo ya pesa taslimu) kama inahitajika na agizo lako wakati bima ya afya haitolewi.

Kama agizo lako la msaada linahitaji mzazi anayelea kutoa bima ya afya au kulipia gharama za matibabu ambazo hazina bima, unaweza kuomba huduma kamili ya kutekeleza msaada wa watoto na:

1. Omba DCS kutekeleza jukumu la mzazi anayelea la kutoa bima ya afya. Huenda DCS ikatekeleza jukumu hilo kulingana na hali ya kesi yako.
2. Omba DCS ikusanye gharama za matibabu zisizo na bima pamoja na malipo mengine, vipunguzi, na malipo kama ilivyofasiliwa katika WAC 388-14A-1020 toka kwa mzazi anayelea.

Kama agizo lako halihitaji mzazi anayelea kutoa bima ya afya, mgao wa pesa za matibabu, au kulipia gharama za matibabu zisizo na bima, kama ilivyofasiliwa katika WAC 388-14A-1020, unaweza kuomba DCS kuhakiki agizo lako la urekebishaji au unaweza kuomba rufaa ya urekebishaji kivyako.

Aina za Rufaa

Bodi ya Mkutano. Bodi ya mkutano ni utaratibu wa usimamizi (usio wa mahakama) unaotumiwa kutatua migogoro mingi, kufafanua sera, na kubainisha kweli.

1. Bodi ya mkutano huenda ikahakiki agizo la mahakama na agizo lisilo la mahakama la kesi za msaada wa watoto.
2. Bodi ya mkutano huenda ikatoa uamuzi bila kukutana na wewe. Kama una mkutano, unaweza kujadili kesi yako na usimamizi wa DCS ambao unaweza kubatilisha maamuzi ya awali ya DCS. Bodi ya mkutano inaweza kubadilisha baadhi ya hatua zilizochukuliwa na wafanyikazi DCS lakini haiwezi kubadilisha hatua zinazohitajika na sheria.

Uamuzi Kesi (usikilizaji). Usikilizaji pia ni utaratibu wa usimamizi (usio wa mahakama). Usikilizaji ni wa kawaida zaidi ya bodi ya mkutano lakini sio rasmi kama hatua ya mahakama.

1. Sheria ya jimbo hutoa tu usikilizaji wa hali zingine. Kama DCS itakupa ilani, ilani hiyo hukuelezea kama una haki ya usikilizaji. Jaji Msimamizi wa Sheria (ALJ) huongoza usikilizaji. ALJ sio waajiriwa wa DCS.
2. Wakati wa usikilizaji, ALJ uhakiki kesi yako na kutoa uamuzi juu ya mzozo wako. Kukomesha DCS dhidi ya kutekeleza agizo lako la msaada wa watoto, lazima uombe usikilizaji kati ya siku 20 (kama ulipokea ilani katika Jimbo la Washington) au kati ya siku 60 (kama ulipokea ilani nje ya Jimbo la Washington) baada ya kupokea ilani hii.
 - a. Unaweza kuomba usikilizaji baada ya kipindi cha siku 20 au 60. Walakini, DCS itatekeleza agizo lako la msaada hadi upokee uamuzi wa usikilizaji. DCS haitarejesha fedha zozote zilizokusanywa wakati unapokuwa ukisubiri uamuzi wa usikilizaji.
 - b. Ukiomba usikilizaji zaidi ya mwaka mmoja baada ya kupokea ilani yako, utahitajika kuonyesha sababu nzuri (sababu nzuri ya kufanya ombi kawizo). ALJ haiwezi kukupa ombi lako kawizo. Walakini, huenda ukawa na haki ya kurekebisha jukumu lako la usoni la msaada wa watoto hata kama huna sababu nzuri ya ombi la usikilizaji kawizo.
3. Utatumiwa nakala ya uamuzi wa ALJ. Uamuzi wa ALJ utakuwa na maelezo kuhusu haki zako za kuomba rufaa.
4. Kama inafaa, DCS itaelezea wahusika wote wa agizo lako wakati tunapokea ombi la usikilizaji. Wahusika wote wanaweza kuhusika katika usikilizaji.

Kama una maswali:

DIVISION OF CHILD SUPPORT

PO BOX 11520

TACOMA WA 98411-5520

Katika eneo _____ la kupiga simu _____

Nje ya eneo _____ la kupiga simu _____

Huduma za TTY/TDD zinapatikana kwa walio na ulemavu wa kuongea au kusikia.

Tembelea tovuti yetu iliyo: www.dshs.wa.gov/esa/division-child-support

Hakuna mtu yeyote kwa sababu ya umbari, asili ya kitaifa, imani, dini, jinsia, umri, au ulemavu, anapaswa kubaguliwa katika ajira, huduma, au hali yoyote ile ya shughuli za mpango huu. Fomu hii inapatikana katika fomati tofauti ukiomba.